

Habari kuhusu COVID-19

Kazi ya ACLU ya Idaho ni kudhibiti haki za kiraia na za uhuru. Kusambaa kwa ugonjwa wa COVID-19 hakujabadilisha kazi hiyo. Tume kuwa tukifuata yanayo endelea hapa Idaho kwa sababu ya COVID-19. Tume tuma barua kwa Gavana, Idara ya Marekebisho na Idara ya Marekebisho ya Vijana pamoja na jela, sheriff, polisi na hakimu tukiwaomba waachilie mara moja watu walio kwenye jela na gerezani, waache kuwanasa watu na kuwatia jela na kudhibiti wale ambao wanaeza shikwa na virusi. Watu hawa ni pamoja na wafanyi kazi, wahamaji na wanao husika na mfumo wa kisheria wa jinai.

ACLU ya Idaho ina amini kwamba:

- Ina bidi jawabu lolote la COVID-19 liwe na msingi wa kisayansi na wa afya ya umma
- Mpango wowote wa jawabu lazima udhibiti afya, usalama na uhuru wa kiraia kwa wote.
- Ita bidi viongozi wa serikali waombe watu wakae nyumbani kama vile inavyo wezekana
- Ita bidi viongozi wa wasaidie walio hatarini kwenye jamii yetu kama wanataka kusaidia kusimamisha kusambaa kwa virusi

Watu walio kwenye jela, gerezani, jela za vijana na hospitali za serikali

Watu walio jela na gerezani wana uhatari mkubwa wa kushikwa na ugonjwa. Viongozi wa jimbo na wanasheria wa mtaa wangewaachilia watu ilikusaidia virusi kutoingia gerezani au kwenye jela.

Waite viongozi wa serikali na uwahimize waachilie watu wengi iwezekanavyo mara moja. Waombe pia waache kunasa watu mara moja na kuwatia kwenye jela.

Gavana Brad Little: 208-334-2100

Mahakama Kuu ya Idaho: 208-334-2210

Pia muite sheriff wa mtaa wako, kamishna wa kata na diwani. Tafuta namba zao kwenye mtandao.

Hapa chini pana habari zaidi ya kujulisha wapendwa wako walio gerezani, jela, jela za vijana na kwenye hospitali za serikali.

Wahamiaji

Pasiwe na mtu anaye ogopa kupata matibabu kwa sababu anaogopa kunaswa. Idara ya uhamiaji na forodha ya Marekani (ICE) yasema kwamba haita wanasa watu kenye kliniki za matibabu. ACLU imewaomba ICE wakomeshe kuwanasa ilikutia kikomo virusi kusambaa kwenye jela na vituo vya vizuizini.

Kufukuzwa

Tangu mwezi wa Machi tarehe 27 mwaka wa 2020 hadi mwezi wa Aprili tarehe 15 mwaka wa 2020 kufukuzwa kwa wapangaji kumesimamishwa. Mahakami Kuu ya Idaho ilitowa amri ya dharura. Kufukuzwa kwa wapangaji kutaendelea tu kama dawa za kulevya zina husika kwenye nyumba hiyo.

ACLU ya Idaho imejiunga na wengine kwa madai ya kukomesha kufukuzwa kwa wapangaji kwenye jimbo nzima. Kufukuza watu kutoka nyumba zao wakati kuna amri ya kukaa nyumbani ni kukataa akili ya kawaida na pendekezo za afya ya umma.

Kuna sheriff wengine wa Idaho ambao wanaeza kuwa bado wana lazimisha watu kutoka nyumba zao kulingana na amri za kufukuzana zilizo tolewa kabla mwezi wa Machi tarehe 27 mwaka wa 2020. Ita sheriff aliye karibu na umuombe kama amri za kufukuzwa zinaweza simamishwa kwa sasa. Unaweza tafuta nambari ya sheriff aliye karibu kwenye mtandao.

Habari zaidi kuhusu watu walio kwenye jela na gerezani na wapendwa wao

Tuna jaribu kuwahimiza viongozi wa serikali wafanye kilicho cha usalama na kilicho sawa na kuwaachilia watu pia. Tuna jaribu kuwahimiza viongozi wa serikali waache kuwanasa watu na kuwafunga jela kwa sasa. Tuna waomba gavana pamoja na Idara ya Marekebisho, sheriff, waendesha mashtaka na polisi kuwaeka watu wakiwa salama kwa kuwatoa na kuwazuia kutokuwa gerezani na kwenye jela.

Dalili za COVID-19 ni kuchemka mwili, kikohozi na upungufu wa pumzi.

Ili kukomesha kusambaza kwa viini itabidi gereza na jela zihakikishe kwamba unaweza fanya vitu vitano vifuatavyo:

1. Kuto karibiana na watu walio wagonjwa.
2. Funika mdomo wako na tishu unapo kohoa au kutoa chafya, kisha uitupe kwenye takataka.
3. Jiepushe kuguza macho yako, pamoja na pua na mdomo.
4. Safisha na utakase vyombe pamoja na sehemu unazo guza.
5. Safisha mikono yako mara nyingi kwa kutumia maji na sabuni kwa angalao sekunde 20.

Unaeza tusaidia kufuatilia yanayo endelea kwenye jela na gerezani kwa wakati huu. Tafadhali tujulishe kama hauwezi fanya yoyote kati ya hivi vitu vitano. Tafadhali tujulishe ukiwa na shida zozote kati ya hizi:

- Haupati sabuni au kitakasa au bidhaa vya usafi vya kutosha
- Inabidi ugharamiye iliupate matibabu
- Kujihisi ukiwa na dalili za COVID-19 bila kukaguliwa na kupimwa.
- Kuwekwa pamoja na au kufanya kazi na watu walio na dalili za COVID-19 au walio patikana wakiwa nao.
- Kutoweza kuongea na familia, wapendwa wako au wakili

Unaweza kutujulishe kuhusu shida za COVID-19 zilizo kwenye jela na gerezani kwa kufikisha malalamishi kwa <https://intake.acluidaho.org> au kutuma barua kwa:

ACLU of Idaho
P.O. Box 1897
Boise, Idaho 83701

Ukiwa jela, gerezani au kwenye hospitali ya serikali hakikisha kwamba umetia alama ya “LEGAL MAIL” na “CONFIDENTIAL” ndani na nje ya barua yako.

Pia unaweza ongea na mtetezi wako wa umma au wakili wa jinai na uwaulize waombe mahakama ikuachiliye kwa sababu ya virusi vya korona.